

## Mwongozo wa SNAP kwa Familia



### Msaada wa Nyongeza ya Lishe

**Mpango (SNAP)**, ambao zamani ulijulikana kama Food Stamp, husaidia watu binafsi na familia kuweka chakula mezani. SNAP ni programu bora zaidi ya taifa, kuwaweka Wamarekani milioni 8 kutoka kwa umaskini, ikiwa ni pamoja na watoto milioni 4. Zaidi ya watu 900,000 wa Tennessee wanategemea SNAP kuepuka njaa.

### Stahili ya kupata SNAP

Kustahili kupata SNAP kunatokana na mapato na rasilimali zako. Ni lazima kaya yako iwe na rasilimali zisizozidi \$2,250, kama vile akiba. Mapato ya kaya yako lazima yawe chini ya kiwango cha mapato kilichoordheshwa hapa chini.

Kaya zilizo na mtu aliye na umri wa zaidi ya miaka 59 au anayefaidika na msaada kwa wasiojiweza, anaweza kufaidika, hata kama wana rasilimali au mapato zaidi.

Ukubwa wa Kaya	Mapato ya Kila Mwezi
1	\$1,383
2	\$1,868
3	\$2,353
4	\$2,839

Mbali na kukidhi mahitaji ya mapato, familia zinaweza kustahiki iwapo zitatimiza angalau mojawapo ya vigezo vifuatavyo:

- Wanapokea msaada wa Muda kwa Familia zenye uhitaji (TANF -Temporary Assistance for Needy Families)/Familia Kwanza au Social security(SSI)
- Matunzo ya mtoto chini ya umri wa miaka 18
- Mwanakaya ambaye ni mjamzito

Ikiwa wanakaya wote wako kati ya umri wa miaka 18-49, angalia mahitaji ya ziada hapa:

<https://bit.ly/SNAPABAWD>

Piga 211 itachunguzwa ili kubaini ustahiki

### Ninaweza kupata kiasi gani?

Kiasi cha faida cha SNAP kinategemea mapato yako, gharama, na idadi ya watu katika kaya yako. Tennessee, kiwango cha juu cha manufaa ya kila mwezi kwa mtu binafsi ni \$204. Kiwango cha wastani cha faida ya kila mwezi ni \$150. Faida huwekwa kwenye kadi ya Electronic Benefit Transfer (EBT) kila mwezi.

### Kadi ya EBT inafanya kazi vipi?

Kadi ya EBT hufanya kazi kama kadi ya malipo na inakubalika katika takriban maduka yote ya mboga na maduka makubwa. Inaweza kutumika kununua chakula na kwenda kupikia nyumbani. Unaweza kununua mbegu za mboga mbalimbali na mboga za majani ambazo unaweza kula.

Masoko mengi ya wakulima sasa yanakubali SNAP. Baadhi ya masoko hutoa "pesa za bonasi" za kutumia kwenye mazao mapya ikiwa unatumia kadi yako ya EBT. Angalia soko lako la karibu kuhusu fursa hii.

### Omba SNAP

Omba kupitia kwenye mtandao:

<https://onedhs.tn.gov/csp>

Tuma maombi kwa njia ya fax au barua kwenye ofisi ya Department of Human Services (DHS) kwenye ofisi ya county. Tafuta ofisi ya county yako:

<https://bit.ly/SNAPOffices>

Piga simu DHS kwa maelezo zaidi: 1-866-311-4287

### Mchakato wa Maomba

Ni bure na ni siri.

Ukituma maombi kwa njia ya mtandaoni inachukua kama dakika 30.

Maombi lazima yawasilishwe katika Ofisi ya DHS katika county ya makazi ya mwombaji.

Jiandae kutoa taarifa ya mapato (mshahara, pesa kutoka kwa wazazi), gharama (kodi, huduma, gharama za malezi ya watoto), na rasilimali (maelezo ya akaunti yako ya benki). Nyaraka zinazounga mkono ni muhimu (mfano ni pamoja na, le karatasi za mshahara, kodi ya nyumaba, nk).

Mahojiano na mfanyakazi wa DHS- caseworker yatapangwa baada ya karatasi zako kuwasilishwa. DHS ina siku 30 kushughulikia ombi lako.

Piga simu Kituo cha Haki cha Tennessee 877-608-1009 iwapo utakuwa na tatizo wakati wa kujaza maombi yako.